(3)

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

## MKATABA WA KUKODISHA GARI-FUSO KWA AJILI YA KUSAFIRISHA VIFAA VYA UJENZI-WHITE CEMENT, BIDHAA ZA CHUMA,MIKANDA YA GYPSUM

## KWA AJILI YA UJENZI WA CHUO CHA VETA RUFIJI

**MKATABA NA: PA/24/2021/2022/TRA/RUF-14**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe **23** mwezi **03 - 2022**

**KATI YA**

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha **PWANI, S.L.P. 30345, KIBAHA, PWANI** ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

**NA**

**M/S PASCHAL & SONS TRANSPORT COMMUSION AGENT wa S. L. P.70981 DAR ES SALAAM.** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni wa usafirishaji vifaa ") kwa upande mwingine.

**KWA KUWA** Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFIJI;

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFIJI;

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya RUFIJI ambayo ujenzi wake unaendelea;

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

1. **GHARAMA ZA USAFIRISHAJI**

   Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania **1,600,000/=** kwa kuasafirisha vifaa vya ujenzi kutoka Dar es Salaam mpaka eneo la ujezi Utete Rufiji kama inavyoonekana kwenye jedwari hapo chini kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu,kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama za usafirishaji vifaa vya ujenzi"

Gharama za kazi zitakazofanyika katika kila jengo ni kama ifuatavyo:

| S/N | | STAGE | BEI ILIYOKUBALIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | | GHARAMA ZITAKAZOTUMIKA KUSAFIRISHA VIFAA VYA UJENZI-WHITE CEMENT, BIDHAA ZA CHUMA,MIKANDA YA GYPSUM KUTOKA KAMAKA KWENDA ENEO LA UJENZI UTETE RUFIJI | **1,600,000** |
| | | | |
| | JUMLA | | **1,600,000** |

## 2. MABADILIKO YA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI (*TRANSPORTATION SUM ADJUSTMENT*)

Gharama za usafirishaji hazitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko yoyote yaliyofanywa na Mwajiri.

## 3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Malipo yatafanyika baada ya kazi kukamilika yaani Mzigo kufika eneo la ujenzi ukiwa salama na kwa idadi na kiwango kilichotakiwa.

•

## 4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

(a) Mzabuni wa usafirishaji atakabidhi mzigo kwa wahusika wakuu waliopo eneo la ujenzi na kusainisha hati za mapokezi na nyaraka zingine muhimu kuonesha uhalali wa mapokezi ya mzigo husika.

(b) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Mzabuni wa usafirishaji kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo pasipo kuathiri pande zote.

## 5. WAJIBU WA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kusafirisha mzigo wa vifaa vya ujenzi kwa kadri alivyokubaliana katika mkataba sambamba na maelekezo ya Mwajiri.

(b) Kumjulisha Mwajiri kuhusu mapungufu au mkanganyiko wowote utakaobainika

Katika ubebaji wa vifaa hivyo.

(c) Kuhakikisha usalama wa Vifaa vya ujenzi unafika vizuri katika eneo la ujenzi.

(d) Kuzingatia na kutekeleza masharti yote ya Sheria za nchi zinazohusiana na kazi ya usafirishaji mizigo

(e) Kukubali kukatwa na Mwajiri kodi ya zuio (withholding tax).

(f) Gari ikiharibika ni juu ya mzabuni kutengeneza mwenyewe.

## 6. WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kumlipa Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi malipo halali ya kazi iliyoainishwa katika Mkataba huu kulingana na utaratibu uliobainishwa katka kipengele Na.3 cha Mkataba huu, pale Mzabuni wa usafirishaji atakapokuwa ametimiza wajibu wake kikamilifu kulingana na Mkataba huu.

(b) Kutoa idhini/kibali cha kuanza kazi kwa mzabuni

(g) Kuzingatia na kutekeleza masharti yote ya Sheria za nchi zinazohusiana na kazi
(h) husika.
(c) Kumkata Mzabuni wa usafirishaji wa vifaa vya ujenzi kodi ya zuio (withholding tax).

## 7. MSIMAMIZI WA UJENZI (PROJECT SUPERVISOR)

(a) Mwajiri atakuwa na haki ya kuweka Msimamizi wa Ujenzi (*Site Supervisor*), ambaye atakuwa na jukumu la kufanya uhakiki wa shughuli za ujenzi,kupokea vifaa vya ujenzi akisaidiana na kamati ya mapokezi kwa niaba ya Mwajiri, na Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi atatoa ushirikiano wote kwa Msimamizi wa Ujenzi (*Project Supervisor*) au Mwakilishi wake katika kutimiza majukumu yake.

(b) Msimamizi wa Ujenzi (*Site Supervisor*) akisaidiana na Mtunza Stoo ndio watakuwa wapokeaji wakuu wa vifaa vya ujenzi husika.Mzabuni anapaswa kuonana na wahusika hao kwa taratibu zote za kukabidhiana vifaa hivyo.

## 8. NOTISI *(NOTICES)*

Mawasiliano yote, Hati, Notisi yatakayofanyika katika Mkabata huu, yatafanyika kwa ama kupelekwa moja kwa moja(physically) kwa upande wowote wa Mkataba au kupitia anwani ya posta kwa barua iliyosajiliwa (registered mail).

## 9. SHERIA ZINAZOTUMIKA

Sheria za kutafsiri Mkataba huu na ufanyaji wa kazi katika Mkataba huu ni Sheria za Tanzania.

## 10. RUSHWA

Iwapo Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi, watumishi au wasaidizi wake katika kutekeleza majukumu haya kama kujihusisha na masuala yoyote ya rushwa ama jinai yoyote, basi Mwajiri anaweza kuvunja Mkataba huu.

## 11. KUVUNJWA KWA MKATABA

Mkataba huu unaweza kuvunjwa na upande wowote wa Mkataba huu.

(a) Mkataba kuvunjwa na Mwajiri:
Bila ya kuathiri haki zozote za Mwajiri, iwapo Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi akifanya makosa yafuatayo:

i. Kutopakia na kusafirisha vifaa kwa muda wa makubaliano

ii. kutofuata maelekezo sahihi ya Mwajiri

## 12. USIRI

Nyaraka zote zitakazokuwa zimetumika katika usafirishaji wa vifaa unaohusu Mkataba huu hazitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa kazi unayohusu Mkataba huu. Pia taarifa yoyote itakayopatikana wakati wa kazi inayohusu Mkataba huu haitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa kazi inayohusu Mkataba huu.

## 13. USULUHISHI WA MIGOGORO

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhisha mgogoro, basi upande wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi(arbitration).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA PWANI (PWANI RVTSC)

Jina: CLARA KIBODYA Saini: ______________

Wadhifa: KAIMU MKUU WA CHUO Tarehe: 23/03/2022

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: LUKA C. MKINI Saini: ______________

Wadhifa: M/KITI KAMATI YA UJENZI Tarehe: 23/03/2022

IMESAINIWA NA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

**Mbele ya**

Jina: PASCHAL RAINI Saini: ______________

Wadhifa: DIRECTOR Tarehe: 23-3-2022

REGIONAL VOCATIONAL TRAINING & SERVICE CENTRE
PAID
23 MAY 2022
KIBAHA
PWANI

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: JULIUS JONAS Saini: ______________

Wadhifa: SECRETARY Tarehe: 23-3-22